

Kadi ya Chanjo ya COVID-19 / MyIR Mobile Maswali Yanayoulizwa Mara kwa mara

Kadi ya Chanjo ni nini?

Vax Card (Kadi Chanjo) ni rekodi rasmi ya chanjo yako ya COVID-19. Wakati wa chanjo, unafaa kuwa umepokea kadi kutoka kwa CDC (Kituo cha Udhhibiti na Uzuiaji wa Magonjwa) iliyo na tarehe zako na chapa ya chanjo ya COVID-19. Ikiwa hukupokea kadi au ulipoteza kadi yako, kuna njia nyingine za kuthibitisha kuwa umepokea chanjo (tazama maswali na majibu yanayofuata).

Nini inafuzu kuwa rekodi rasmi ya chanjo?

Ifuatayo ni mifano ya rekodi rasmi za chanjo:

- Rekodi ya chanjo ya milele/CDC Kadi ya Chanjo ya COVID-19
- Jimbo la Washington Immunization Information System (Mfumo wa Taarifa ya Chanjo) uliochapishwa
- [MyIR](#) (Kiingereza pekee) iliyochapishwa (ama picha ya skrini au Cheti cha Hali ya Chanjo)
- [My IR Mobile](#) (Kiingereza pekee) Cheti cha Chanjo ya COVID-19
- Chapisho la rekodi ya matibabu ya kieletroniki iliyothibitishwa kutoka kwa mtoaji wako wa huduma ya afya

Huwezi kujiundia Kadi ya Chanjo, kwani haitakubaliwa kama rekodi rasmi. Rekodi rasmi ni nyaraka za matibabu zilizothibitishwa ambazo zinapatikana wakati wa chanjo, kupitia kwa mhudumu wako wa afya, au kupitia vituo vya huduma za MyIR vilivyoorodheshwa hapo juu.

Nafaa kuhifadhi Kadi yangu ya Chanjo kwa njia gani?

Unafaa kuweka Kadi yako ya Chanjo katika eneo salama! Chukulia hii kana kwamba ni cheti chako cha kuzaliwa au pasipoti. Unaweza kuipiga picha, kurudufisha nakala, kuongeza safu kwenye nakala hiyo (lakini si nakala asili), au kuchukua hatua nyingine kuhakikisha kuwa una nakala zake.

Kwa vidokezo zaidi kuhusu kushughulikia Kadi yako ya Chanjo vizuri, unaweza kushiriki hii na familia ya marafiki. Bofya hapa kwenye bango katika lugha yako: (kwa sasa linapatikana katika [Kiingereza](#) na [Kihispania](#)).

Kwa nini nahitaji kuhifadhi Kadi yangu ya Chanjo?

Kadi yako ya Chanjo ni njia rahisi kwako kuonyesha uthibitisho kuwa umepewa chanjo dhidi ya COVID-19. Unaweza kuhitaji kuonyesha uthibitisho wa chanjo ili kuweza kusafiri, kuhudhuria matukio fulani, na kuweza kuongeza taarifa ya dozi ya kuimarisha kinga baadaye.

Biashara nyingi za Washington sasa pia zinatoa vichochezi kwa wanaotoa uthibitisho uliothibitishwa wa chanjo kamili. Hii inaweza kujumuisha vipunguzo, bidhaa ya bure au viti unavyopendelea kwenye matukio.

Nifanye nini ikiwa sikupata Kadi ya Chanjo wakati wa kupata chanjo yangu?

Ikiwa hukupata Kadi ya Chanjo ulipopata chanjo zako za COVID-19, unaweza kuwasiliana na mtoaji wako wa chanjo. Unaweza pia kufikia rekodi zako za chanjo ya COVID-19 mtandaoni kupitia www.MyIRMobile.com (Kiingereza pekee) na kufungua akaunti ya bila malipo.

Nifanye nini ikiwa nilipoteza Kadi yangu ya Chanjo?

Ikiwa ulipoteza Kadi yako ya Chanjo, unaweza kupata uthibitisho rasmi wa chanjo ya COVID-19 kupitia mhudumu wako wa afya au kwa kufungua akaunti www.MyIRMobile.com (Kiingereza pekee).

MyIR Mobile ni nini?

MyIR Mobile ni kituo kinachoegemea intaneti na huwapa watu ufikiaji wa rekodi zao rasmi za chanjo za jimbo. Unaweza kufungua akaunti katika www.MyIRMobile.com (Kiingereza pekee).

Tafadhali kumbuka kuwa MyIR Mobile kwa sasa imewekewa kikomo kwa lugha ya Kiingereza pekee. Kwa ajili ya usaidizi wa lugha, au usaidizi wa ziada wa kupata rekodi zako, unaweza pia kupigia Office of Immunization and Child Profile (Ofisi ya Chanjo na Wasifu wa Mtoto) katika Jimbo la Washington wakati wa saa za kawaida za biashara kupitia (360) 236-3595 au wasiliana kwa barua pepe kupitia waisrecords@doh.wa.gov.

Nitapataje rekodi ya chanjo ya COVID-19 ya mtoto wangu?

Mtoto wako anafaa kuwa alipokea Kadi yao ya Chanjo ya CDC mara tu alipopokea chanjo. Ni wazo zuri kuwa uweze kuhifadhi kadi hii salama kwa ajili yao kwa njia sawa unayohifadhi kadi yako. Tazama orodha ya chaguo za uhifadhi hapo juu.

Ikiwa mtoto wako hana Kadi ya Chanjo ya CDC, unaweza kupata nakala rasmi kupitia daktari wao wa watoto au mtoaji wa chanjo. Unaweza pia kufungua akaunti ya familia kwenye www.MyIRMobile.com (Kiingereza pekee) na kuongeza wasifu wa mtoto wako wewe binafsi.

Je, na ikiwa nilipokea chanjo nje ya jimbo la Washington?

Ikiwa hukupokea chanjo katika jimbo la Washington, rekodi zako za chanjo huenda zisiakisiwe kwenye MyIR Mobile. Tafadhali hakikisha kuwa una uthibitisho mwingine uliothibitishwa wa chanjo ya COVID-19, kama vile Kadi yako ya Chanjo ya CDC au rekodi nyingine zilizothibitishwa kupitia kwa mhudumu wako wa afya.

Ikiwa hukupokea chanjo Marekani, tafadhali beba uthibitisho rasmi wa chanjo kutoka kwa nchi uliyopokea chanjo.

Nitapataje rekodi zangu zote za chanjo kwa ajili yangu au familia yangu (si tu chanjo ya COVID-19)?

Kwa orodha yako kamili ya rekodi za chanjo zako ama za familia yako, unaweza kuwasiliana na mhudumu wako wa afya au kufungua akaunti katika wa.MyIR.net (Kiingereza pekee).

Kwa ajili ya usaidizi wa lugha, au usaidizi wa ziada wa kupata rekodi zako, unaweza pia kupigia Office of Immunization and Child Profile (Ofisi ya Chanjo na Wasifu wa Mtoto) katika Jimbo la Washington wakati wa saa za kawaida za biashara kupitia 360-236-3595 au wasiliana na barua pepe kupitia waisrecords@doh.wa.gov.



DOH 348-819 June 2021

Ili kuomba waraka huu katika muundo mwingine, piga simu 1-800-525-0127. Wateja ambao ni viziwi au wasio na uwezo wa kuzungumza, tafadhali piga simu 711 ([Washington Relay](http://WashingtonRelay.com) (Kiingereza)) au tuma barua pepe civil.rights@doh.wa.gov.